

**Nyimbo:** Nzela

**Waimbaji:** Banana Zorro and the B-Band

**Video URL:** <http://www.youtube.com/watch?v=hxi-9550q8Y>

### **Maana ya maneno (words and expressions explained)**

Mwana – child/daughter or son

Kupiga simu – to make phone call

Umetoroka (kutoroka) – to run away

Kisa – reason

Hata – even

Hawajui (kujuia) – to know

Zimetapakaa (kutapakaa) – to be spread

Ujauzito (mjamzito) – pregnant

Ulopewa (kupewa) – to be given

Mpiga debe – bus conductor

Anakuita (kuita) – to call

Akuone (kuona) – to see

Rudi (kurudi) – to return

Tunakutafuta (kutafuta) – to look for

Unampa (kupa) – to give

tabu – worries/troubles

Tabia – behavior

Tambara – old piece of cloth

Lililotoboka (kutoboka) – to pierce

Naumia (kuumia) – feel pain/get hurt

Kumbuka – to remember

### **Maswali (Questions)**

1. Nyimbo hii inahusu nini?
2. Kwanini Nzela alitoroka nyumbani?
3. Unafikiri Nzela alikimbilia wapi?

4. Ni nani anamtafuta Nzela?
5. Unafikiri ni gonjwa gani zito linalozungumziwa kwenye nyimbo hii?

### **Mazoezi (Exercises)**

1. **Sikiliza nyimbo kwa makini halafu jaza mapengo:**

Dada kanipigia \_\_\_\_\_ eti, umetoroka nyumbani, hawajui hata kisa nini ee, hata kisa nini,

\_\_\_\_\_ zimetapaka mjini, una \_\_\_\_\_, Ulopewa na mpiga debe ee,  
na mpiga debe,

Nzela mama mama anakuita mwana, \_\_\_\_\_ nyumbani mama akuone mwana,  
Nzela mama mama anakuita mwana, mama akuone mwana.

### **Kiitikio:**

Ooo Nzela x 8

Nzela dada yangu rudi \_\_\_\_\_, sisi tunakutafuta, nipo hapa na mjomba yetu  
Nzela, Nzela,

\_\_\_\_\_ wawili Nzela Nzela, juu mama unampa \_\_\_\_\_ Nzela Nzela,  
*We miss u, Nzela Wela yoo mamama Nzela x 2*

### **Kiitikio:** oooo Nzela

Nzela mimi \_\_\_\_\_ yako Nzela, nimesoma na kaka yako Nzela, naumia na  
\_\_\_\_\_ ulonayo, kumbuka \_\_\_\_\_ shule we mama, dunia  
ni tambara lililotoboka, kumbuka kuna \_\_\_\_\_ zito Nzela.

### **Kiitikio:** ooo Nzela

*Come back x 2, come back Nzela, Nzela wetu,*

*Nzela mama miss you, Nzela wa mama, your brothers and sisters miss you, Nzela wetu, come back Nzela, come back home*

*Come back, come back x 6*

**Kiitikio:** ooo Nzela

2. Unafikiri kisa cha nyimbo hii kinaweza kutokea hapa Marekani? Kwanini?
3. Tayarisha mchezo wa kuigiza juu ya nyimbo hii.
4. Andika sentensi zenyeh maana kwa kutumia maneno yafuatayo:
  - i. Kutoroka
  - ii. Kupiga simu
  - iii. Tabia
  - iv. Kutapakaa
  - v. Kisa
  - vi. Tabu
  - vii. Kumbuka